



MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI



CHUO CHA UALIMU WA UFUNDI STADI MOROGORO (MVTTC)

TANGAZO LA NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU WA UFUNDI NA UFUNDI STADI DIRISHA LA MWEZI SEPTEMBER, MWAKA WA MASOMO 2023/2024



1.0. UTANGULIZI

Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTTC) kilianzishwa 1997 na sheria ya Bunge (VET Act. 1994) (CAP 82, Rejeo la 2006, 2009, na 2021). MVTTC ni Chuo kilichosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), kwa namba za ujasajili REG/BTP/128 kama Chuo cha Ufundi chenye kutoa Mafunzo ya Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi.

2.0 UDAHILI

MVTTC inakaribisha maombi ya udahili kwa kozi za Ualimu wa Ufundi na Ufundi Stadi kupitia **dirisha la mwezi Septemba**, mwaka wa masomo **2023/2024**.

UFUNDI STADI KWA AJIRA NA MAENDELEO YA VIWANDA

VETA MAKAO MAKUU

Kiwanja Na. 18, Central business Park (CBP)
S. L. P. 802,
DODOMA.

+255 755 267 489

VETA   

SIFA ZA UJUMLA KWA WAOMBAJI

Muombaji lazima awe amehitimu fani za ufundi katika sekta za ufundi: Vyuma; Umeme; Ujenzi; Magari na Mitambo; Huduma za Biashara; Nguo na Mavazi; Usafirishaji; Uziduzi (Madini, Mafuta na Gesi); Uchapaji; Urembo; Kilimo na Usindikaji Chakula; Hoteli na Utalii; Sanaa za mikono na Maonesho.

2.1 STASHAHADA YA UALIMU WA UFUNDI NA UFUNDI STADI (ORDINARY DIPLOMA IN TECHNICAL AND VOCATIONAL TEACHER EDUCATION) –NTA LEVEL 6)

SIFA ZA KUJIUNGA

Muombaji awe na Stashahada ya Ufundi katika Sekta za Ufundi, sawa na 'Ordinary Diploma' (NTA Level 6) au sifa linganishi zinazotambulika na Mamlaka za urekebu na ithibati.

MUDA WA MASOMO

Muda wa masomo kwa kozi hii utakuwa **Miaka 2 (Miezi 24)**.

2.2 CHETI CHA WALIMU WASAIDIZI WA UFUNDI STADI (CERTIFICATE OF ASSISTANT VOCATIONAL TEACHER)

SIFA ZA KUJIUNGA

Muombaji wa kozi hii anatakiwa awe na:

i) Cheti cha Elimu ya sekondari (CSEE) chenye ufaulu usiopungua masomo mawili, bila kujumuisha masomo ya dini.

ii) Cheti cha Ufundi Stadi Ngazi ya 3 (National Vocational Award Level III) au Cheti cha Majaribio ya Ufundi Stadi Daraja la Kwanza (Trade Test Grade One (au sifa linganishi inayotambulika na Mamlaka za urekebu na ithibati.

MUDA WA MASOMO

Muda wa masomo kwa kozi hii utakuwa **mwaka mmoja (Miezi 12)**.

3.0 MFUMO WA UJIFUNZAJI

3.1 Kuhudhuria mafunzo ya ana kwa ana chuoni - MVTTC

3.2 Kujifunza kwa njia ya masafa (elimu mtandao) kupitia vituo vya:

i. Kanda ya Kaskazini - (VETA Moshi).

ii. Kanda ya Ziwa - Lake Victoria Disability Vocational Training Centre (LVDC) - Msoma, VETA Mwanza & VETA Kagera)

iii. Kanda ya Kati - (VETA Dodoma).

iv. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - (VETA Iringa & VETA Mbeya)

v. Kanda ya Dar es Salam - (VETA Dar es Salaam).

vi. Kanda ya Magharibi - (VETA Tabora & VETA Shinyanga)

4.0 ADA ZA MAFUNZO KWA KILA KOZI

Maelezo zaidi kuhusu muundo wa ada yanapatikana katika tovuti ya chuo www.mvttc.ac.tz.

UTARATIBU WA MAOMBI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO

1. Fomu za kujiunga zinapatikana chuoni MVTTC Barara ya Rwegasore Manispaa ya Morogoro au fomu zinaweza kupakuliwa katika tovuti ya VETA na MVTTC: www.veta.go.tz au www.mvttc.ac.tz.

2. Kwa maelezo zaidi na ufafanuzi kuhusu udahili tafadhali piga simu kupitia Namba **0682 29 20 94, 0754 59 01 53** na **0765 19 19 19**.

3. Fomu ya maombi iliyojazwa kwa usahili iwasilishwe Chuoni MVTTC kwa mkono au itumwe kwa **barua pepe mvttc@veta.go.tz kabla ya tarehe 30 Septemba 2023** . Fomu za maombi ziambatanishwe na **malipo ya fomu ya gharama ya Shilingi 10,000 tu**.

4. Malipo yafanyikwe kwa kutumia Namba za malipo (control number) zinazopatikana Ofisi za Uhasibu Chuoni au tumia Benki ya CRDB au NMB.

Tangazo hili limetolewa na;

**MKUU WA CHUO,
CHUO CHA UALIMU WA UFUNDI STADI MOROGORO (MVTTC).**

**S.L.P 671,
MROGORO, TANZANIA**

TEL: +255 23 2614466

FAX: +255 23 2614466

EMAIL: mvttc@veta.go.tz

WEBSITE: www.mvttc.ac.tz